



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



Tarehe 14/11/2023

**TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA KWA AJILI YA UJENZI WA MIUNDO
MBINU YA HOSPITALI YA WILAYA YA RUNGWE KATIKA JENGO LA WAGONJWA
WA NJE (OPD)**

ZABUNI NA:LGA/071/2023/2024/RDC/CS/03

14. **Mkurugenzi Mtendaji (W)** anawatangazia Wananchi wote kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imepokea fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa **Miundo mbimu ya Hospital ya Wilaya Wilaya ya Rungwe Katika Jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD)** itakayojengwa katika Kata ya Makandana kupitia **SELIKALI KUU** kwa mwaka wa fedha 2023/2024.
15. Ujenzi wa Miundo mbinu katika Hospital hiyo utahusisha ujenzi wa Wodi la wagonjwa wa Nje OPD pamoja na wodi ya Wanaume na Wanawake.
16. Hivyo basi, Mkurugenzi Mtendaji (W) anakaribisha Mafundi ujenzi wenye sifa na uzoefu katika shughuli za ujenzi wa Miundo mbinu ya Serikali kuomba kazi za Ufundi kwa utaratibu wa "**Force Account**" katika fani na sifa za Ufundi zifuatazo:-

X. Fundi Aluminium

- Awe na uwezo wa kusoma michoro na vipimo vya ramani.
- Awe na uwezo wa kutengeneza madirisha ya Aluminium na milango ya alco bond).
- Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.

XI. Fundi Seremala (inahusisha utengenezaji wa milango na fremu za milango).

- Awe na uwezo wa kutengeneza milango ya mbao ngumu
- Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.

XII. Fundi kuchomelea vyuma (ambao utajumuisha kutengeneza magrill ya milango, madirishana baluster/Hand rail) na bembea za watoto.

- Awe na uwezo wa kutengeneza milango ya "grill", baluster na madirisha

- Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.

17. Pamoja na sifa zilizotolewa hapo juu waombaji wanapaswa kuzingatia masharti kama ifuatavyo:-

- Awe Mtanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea
- Awe na Namba ya Utambulisho wa mlipa kodi (TIN) (aambatanishe na barua ya maombi kwa uthibitisho zaidi)
- Awe na akaunti ya benki kwenye benki yeyote iliyopo ndani ya Rungwe.
- Mwombaji aambatanishe barua ya utambulisho kutoka ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Kitongoji/Mtaa anakoishi.
- Awe tayari kufanya kazi muda wote hadi mradi utakapokamilika

18. Barua za maombi zikiwa zimeambatanishwa na nyaraka tajwa hapo juu ziwasilishwe ofisi ya Mhanga Mfawidhi, Hospital ya Wilaya ya Rungwe, S.L.P 148, Tukuyu yakiwa yamefungwa kwenye bahasha nyuma ya bahasha ikitaja jina la kazi ya Ufundi unaoombwa mfano **Ufundi Seremala n.k**

19. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi za ufundi ni siku ya Jumatatu ya Tarehe 20/11/2023 kabla ya saa 5:00 Asubuhi. Aidha, maombi yatakayoletwa baada ya hapo hayatakubaliwa.

20. Waombaji wote wanatakiwa kuhudhuria usaili wa mafundi wa utakaofanyika tarehe 20/11/2023 saa 6:00 Mchana utakaombatana na kuwashindanisha nukuu za bei za ufundi.

21. Wako katika ujenzi wa Taifa


Juma C. Mwajombe

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE**